

Tanga Cement washirikiki Kili Marathon 2010

Na Mwandishi Wetu, Moshi

KWA mara ya nne mfululizo, Kampuni ya Saruji ya Tanga imefanikiwa kuwa miongoni mwa wadhani ni wakuu wa mbio za Kilimanjaro Marathon 2010.

Wakati wa mbio hizo zilizofanyika juzi mjini Moshi, maofisa wa kampuni hiyo wakiongozwa na Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mipango, Harpreet Duggal walikuwapo mjini hapa.

Akizungunza kabla ya kuanza kwa mbio hizo kwenye Uwanja wa

Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Duggal alisema kampuni yake ni wadun wakubwa wa michezo.

"Tunadhani ni mashindano haya huku tukijivunia kuwa na mipango kamambe ya kuchangia katika kukua michezo nchini. Tunekuwa tukichangia michezo kama mpira wa meza, ngumi na hizi mbio ndefu," alisema Duggal.

Aliweka wazi kuwa udhamini wao kwa mbio hizo ambazo hufanyika mkoani Kilimanjaro unatokana na ukweli kuwa wataja wengi wa saruji ya Tanga wapo katika

mkoa ya Kanda ya Kaskazini, Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga.

Mbali na utadhi huo, kampuni hiyo ilikuwa na washiriki watanu waliokimbia kwenye mbio za nusu marathoni.

Mmoja wa wakimbaji wa kampuni hiyo, Michael Chikona alisema baada ya mbio kumalizika kuwa zilikuwa na ushindani mkubwa.

"Nilikuwa nikifanya mazoezi tangu mwaka jana na nimefurahi kutimiza azima yangu ya kushiriki mbio hizi za umoja," alisema Chikona.

ma.

Alisifia huduma nzuri zilizo kuwa zikitolewa katika vituo mbalimbali wakati wa mashindano ingawa hali ya hewa ilikuwa kikwazo kwake kwani kulikuwa na joto kali katika mwaka jana.

Wakimbaji kutoka Kenya walichukua nafasi za juu kwa qumla na kutawala mbio za mwaka huu huku Steven Chebogut akiibuka mshindi wa mbio ndefu.

Waziri Mkuu Mizengo Pinda ndiye aliyekuwa ngeni rasmi katika tukio hilo lililovuita wengi.